

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI



04 /06/ 2021

## TANGAZO

ZABUNI YA KUTOA HUDUMA YA USAFI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KATIKA JENGO LA UTAWALA LA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI

Halmashauri ya wilaya ya Mbarali inakaribisha maombi ya zabuni ya kutoa Huduma ya Usafi kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 kutoka kwa waombaji wenyewe sifa za kufanya kazi hiyo

### Eneo la Usafi

- a) Jengo la Utawala
- b) Jengo la Maji
- c) Jengo la Ujenzi
- d) Maeneo yanayozunguka ofisi
- e) Mamlaka ya Mji Mdogo

### MASHARTI YA MAOMBI

1. Mwombaji awe na leseni hai ya biashara, TIN, Hati ya usajili, Utambulisho wa kisheria (Power of Attorney) na pia awe na ofisi inayotambulika (Ataje Ofisi ilipo, Anwani, Namba ya simu, Email na Fax kwa ajili ya mawasiliano).
2. Mshindi atapewa mkataba wa kisheria utakaokuwa na masuala yote muhimu ya kuzingatia katika shughuli hiyo ya usafi
3. Mzabuni atatumia mfumo wa kielektroniki kukili mapokezi ya fedha,
4. Waombaji wanaweza kuwa Makampuni, Mashirika au Vikundi vya watu waliosajiliwa kisheria.
5. Mwombaji haruhusiwi kuweka alama yoyote ya utambulisho wake juu ya bahasha.
6. Mwombaji Atatuma maombi kwenye bahasha. Juu ya bahasha iandikwe kwa **HERUFI KUBWA** na zabuni ifungwe kwa **LAKIRI (Seal)** na maombi yakiambatana na kivuli cha stakabadhi ya ada ya maombi yatumwe kwa,

MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI,  
S.L.P 237,  
RUJEWYA – MBEYA.

7. Vitabu nya zabuni kwa lugha ya kiswahili vinauzwa kwa **Tshs.100,000/=** ambazo hazitarudishwa kwa mwombaji na vinapatikana katika ofisi ya Afisa Ugavi (W), **Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, S.L.P 237, RUJEGA –MBARALI.**
  8. Malipo yafanyike kupitia **Benki ya NMB**, Akaunti ya **Own Source Collection**, Akaunti namba **6110000719** baada ya kupewa **Control Number** kutoka kwa mhasibu wa Halmashauri na slip ya bank ilete kwa mhasibu ili kupatiwa risiti kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 09:30 alasiri siku za kazi.
  9. Maelezo ya ziada (masharti) yanapatikana kwenye kitabu cha zabuni husika.
  10. Mwombaji mwenye wafanya kazi wazoefu ambao walisha wahi fanya kazi serikalini au taasisi za serikali kwa kazi hiyo, Kampuni au kikundi kitaambatanisha mikataba au nyaraka zao za malipo alizowahi kufanya kazi hiyo ili kujuwa uzoefu wao
  11. Bodi ya zabuni ya Halmashauri ya wilaya ya Mbarali hailazimiki kukubali au kukataa ombi lolote.
  12. Mwombaji anashauriwa kabla ya kuomba zabuni yoyote kufanya utafiti wa kutosha.
  13. Mwombaji anaweza kuja ofisi za Halmashauri kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kupata ufanuzi atakaohitaji ikiwa ni pamoja na kuonyeshwa maeneo ya kazi.
  14. Mwisho wa kuwasilisha maombi ni **14/06/2022** saa **5:00** asubuhi na zabuni zitafunguliwa siku hiyo saa **5:01** asubuhi katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya. Waombaji au wawakilishi wao wanakaribishwa kuhudhuria siku ya ufunguzi.
- NB;** Vifaa na mali ghafi nya kufanya kazi ni jukumu la Halmashauri

  
Jabir A. Makombe,

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)

**MBARALI.**



---

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Mtaa wa Mpungarelini, S.L.P 237, Rujewa.  
Simu 252957440/252957447, Nukushi 025-2590089/2590108, Barua pepe: [ded@mbaralidc.go.tz](mailto:ded@mbaralidc.go.tz),  
[info@mbaralidc.go.tz](mailto:info@mbaralidc.go.tz), Tovuti: [www.mbaralidc.go.tz](http://www.mbaralidc.go.tz)